

MASOMO YA SEKONDARI KUANZIA ALASIRI (JUMAMOSI KUANZIA ASUBUHI)

Ni kwa wale watakaofanya mtihani wa maarifa (maarufu kama Q.T.) na mitihani mingine ya taifa kama watahiniwa wa kujitegemea. Ebu, bweni la wavulana halina nafasi kwa ajili yao. Pole!

A. KWA WASIOWAHI KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE

Ada ni Tsh. 320,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 500,000, jumla ni Tsh. 820,000. Pamoja na masomo yaliyoorodheshwa hapa chini, wanaohitaji kufundishwa kwa nadharia na vitendo Physics na Chemistry wataongeza Tsh. 80,000 kwa kila somo.

Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019, ila I-II wataanza tarehe 13-11-2018.

**P I: KUJIANDAA MIAKA MIWILI KWA
MTIHANI WA MAARIFA** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics). Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019.

**I-II: KUJIANDAA MWAKA MMOJA
KWA MTIHANI WA MAARIFA** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili). Masomo yao yataanza tarehe 13-11-2018.

**P II: KUJIANDAA MWAKA MMOJA
TENA KWA MTIHANI WA MAARIFA** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana na ile ya kidato cha kwanza. Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019.

**P III: KUJIANDAA MIAKA MIWILI
TENA KWA MTIHANI WA KIDATO
CHA NNE** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics; au Civics, History, Geography, English, Literature na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana na ile ya kidato cha pili. Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019.

**III-IV: KUJIANDAA MWAKA MMOJA
KWA MTIHANI WA KIDATO CHA
NNE** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe wamefaulu mtihani wa maarifa. Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019.

**P IV: KUJIANDAA MWAKA MMOJA
TENA KWA MTIHANI WA KIDATO
CHA NNE** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics; au Civics, History, Geography, English, Literature na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana na ile ya kidato cha tatu na wawe wamefaulu mtihani wa maarifa. Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019.

Tunasisitiza kwamba masomo ya hapo juu (A) si kwa watu wa kurisiti mtihani wa kidato cha nne.

Waliokwishafanya mtihani huo tumejipanga kuwaandaa kurisiti kwa miaka miwili au kwa mwaka mmoja tu kadiri ya hali yao upande wa elimu. Tazama mbele (B).

B. KUJIANDAA KURUDIA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE

Ada ni Tsh. 320,000 kwa mwaka. Wasichana wa bweni wataongeza Tsh. 500,000. Jumla ni Tsh 820,000. Pamoja na masomo yaliyoorodheshwa hapa chini, wanaohitaji kufundishwa kwa nadharia na vitendo Physics na Chemistry wataongeza Tsh. 80,000 kwa kila somo.

**T III na T IV (= TARATIBU):
KUJIANDAA MIAKA MIWILI
KURISITI MTIHANI WA KIDATO
CHA NNE** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics; au Civics, History, Geography, English, Literature na Kiswahili). Masomo yao yataanza tarehe 8-1-2019.

**H (= HARAKA): KUJIANDAA MWAKA
MMOJA KURISITI MTIHANI WA
KIDATO CHA NNE** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili). Masomo yao yataanza tarehe 13-11-2018.

C. KUJIANDAA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA

Ada ni Tsh. 480,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 580,000. Jumla ni Tsh 1,060,000.

**V-VI: KUJIANDAA MWAKA MZIMA
KWA MTIHANI WA KIDATO CHA
SITA** (History, Kiswahili na Language; au History, Geography na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe wamepata credits (A, B au C) walau tatu katika masomo yoyote walipofanya au waliporisiti mtihani wa kidato cha nne. Wawe pia wamepata walau D katika somo la English. Usaili utategemea hati za matokeo ya kidato cha nne tu. Washindi watatangazwa tarehe 2-5-2019 na kuanza masomo tarehe 21-5-2019.

MASOMO YA SEKONDARI KUANZIA ASUBUHI

Ni elimu rasmi kwa wale tu wenye sifa za kufanya mitihani ya taifa kama wanafunzi wa shule. Kwa wengine tuna masomo ya jioni (tazama nyuma).

F I: KUIINGIA KIDATO CHA KWANZA (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics).

Wanaotaka kujiunga wawe wamezaliwa si kabla ya mwaka 2002 na kufaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2017 au 2018.

Usaili utafanyika tarehe 17-11-2018 na 15-12-2018 saa 2:00 asubuhi.

Washindi watatangazwa baada ya siku tatu na kuanza masomo tarehe 2-1-2019.

Ada yao ni Tsh. 480,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wataongeza Tsh. 500,000. Jumla ni Tsh. 980,000.

F V: KUIINGIA KIDATO CHA TANO

(History, Kiswahili na Language; au History, Geography na Kiswahili; au History, Geography na Language; au Chemistry, Biology na Geography; au Physics, Chemistry na Biology).

Wanaotaka kujiunga wawe: wamezaliwa si kabla ya mwaka 1997; wamefaulu kwa alama zisizozidi 25; wamepata credits (A, B au C) katika masomo yote matatu waliyoyachagua walipofanya au waliporisiti mtihani wa kidato cha nne;

wamepata credit ya tatu mwaka 2017 au 2018;

wamefaulu (A, B, C au D) English.

Usaili utategemea vyeti tu (hati za matokeo ya kidato cha nne pamoja na cheti cha kuzaliwa au cha kumaliza shule).

Washindi watatangazwa tarehe 10-6-2019 na kuanza masomo tarehe 2-7-2019.

Ada ni Tsh. 600,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wataongeza Tsh. 500,000. Jumla ni Tsh 1,100,000.

MAELEZO MUHIMU KWA WOTE

Shule yetu ni ya mchepuo wa sayansi.

Pamoja na masomo yaliyoorodheshwa, yale ya Information and Computer Studies, Physical Education na Theatre Art yanafundishwa kwa nadharia na vitendo walau kwa baadhi ya wanafunzi wa asubuhi wa vidato I-IV.

Wale wa vidato V-VI wanafundishwa General Studies na Basic Applied Mathematics kadiri ya maagizo ya serikali.

Mbali na wanaorisiti haraka, Wakristo wa madhehebu yote wanatakiwa kusoma pia Bible Knowledge au Divinity; kwa wengine ni hiari.

Ili kukwepa utapeli na ulanguzi, fomu za kujiunga zinapatikana hapa tu kwa Tsh. 20,000 na zinaweza kununuliwa hata siku ya usaili wa kidato cha kwanza, mradi mhusika alete picha yake ya hivi karibuni au vielelezo vyote vinavyotakiwa.

Inawezekana pia kupakua fomu kutoka tovuti ya shule halafu kulipa shuleni Tsh. 20,000 kwa kuigonga mhuri unaoihalalisha. Usikubali fomu bila mhuri wetu.

Mbali na fomu, malipo yoyote yanatolewa risiti katika ofisi ya mhasibu; nje ya hapo malipo si halali, na shule haihusiki nayo, hata kama aliyepewa pesa ni mwalimu wetu. Jihadhari sana.

Ada zote za bweni na zile za masomo ya asubuhi zinaweza kulipwa kwa mikupuo minne, lakini zile za masomo ya mchana zinatakiwa kulipwa kwa mkupuo mmoja.

Zaidi ya ada hakuna mchango unaodaiwa na shule, ila wanaotarajia kufanya mtihani wa taifa na mitihani mingine inayoagizwa na serikali wajiandae kuilipia kwa wakati wake.

**WANAOHITAJI KUHAMIA
KIDATO CHA PILI, CHA TATU,
CHA NNE AU CHA SITA
TUTAWAELEKEZA SHULE NYINGINE
ZA MTANDAO WETU**

JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO SHULE YA SEKONDARI ALFAGEMS (S.3874)

S.L.P. 6083 – MOROGORO

Tel. 0689-783630 (Ofisi Taaluma)

0689-783672 (Bweni la kike)

0689-782670 (Bweni la kiume)

0789-978886 (Airtel Money)

0752-452444 (mawasiliano M-Pesa)

237405 (uwakala wetu M-Pesa)

www.alfagems.co.tz

Shule yetu inazingatia taaluma na maadili kwa kufuata sera ya elimu ya Kanisa Katoliki.

NAFASI ZA MASOMO

Tunawashukuruni, wananchi wote, kwa kuonyesha mmeipenda sana.

Pamoja na kuwaahidia juhudi endelevu za kuboresha huduma, tunawatangazia nafasi zifuatazo.

Tafadhali, kabla hamjanunua fomu za kujiunga, mtuulize vizuri kuhusu masomo yanayowafaa zaidi.

Baadaye hamtaruhusiwa kubadili fomu wala masomo, kwa sababu ni lazima twende kwa mpango.

Taaluma inadai wanafunzi darasani wasizidi idadi fulani, kumbe msongo wa wanaotaka kusoma kwetu ni mkubwa mno: ndiyo sababu ni lazima pengine tuwachuje sana. Kudai kupokelewa nje ya taratibu zilizopangwa ni kuwadhuru kielimu waliokwisha kubaliwa.

PRE-FORM I: Kwa wanaohitaji kujiandaa miezi mitatu ili kujiunga na shule yoyote, masomo yataanza tarehe 11-9-2018 katika vituo vitatu:

1. Kituo cha Vijana Mt. Elizabeti — Area Six (hakuna bweni)

2. Mtoni-Moro Sekondari — Boma Road (bweni kwa wavulana)

3. Savannah Girls Centre — Mzumbe (bweni kwa wasichana)

Ada ya masomo ni Tsh. 60,000.

Pamoja na bweni ni Tsh. 200,000

